**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA KAGERA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA SERIKALI YA NYAMIYAGA {LUTENI JENERALI SILASI MAYUNGA }

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA**
***Shule ya Sekondari Nyamiyaga, S.L.P 592, Kyerwa***

Namba za simu:
Mkuu wa Shule: 0767 58 36 40 / 0620 670 252
Makamu Mkuu wa Shule: 0746 815 / 0682 088 192
Mwl wa Taaluma :- 0625 101 121 / 0757 433 113
Mganga wa shule { Kwa mambo ya afya tu } 0629 810 609 }
Barua pepe: nyamiyagasecondary@gmail.com

Tarehe …………..

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi
…………………………………………………………………
S. L. P..........................................
........................................................

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYAMIYAGA {LUTENI JENERALI SILASI MAYUNGA} HALMASHAURI YA WILAYA YA KYERWA MKOA WA KAGERA**

**1.0 UTANGULIZI.**

Natumia fursa hii kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Luteni Jenerali Silasi Mayunga { awali ikiitwa Nyamiyaga ss} kidato cha Tano mwaka **…………. Shule yetu ina tahasusi mbili ambazo ni PCB na CBG .** Ninakukaribisha sana nikitumaini kuwa nafasi hii ya pekee utaipokea na kuitumia kwa manufaa yako mwenyewe, wazazi na Taifa kwa ujumla . **KARIBU SANA.**

Shule ya Sekondari Luteni Jenerali Silasi Mayunga ipo katika Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, ipo upande wa Kaskazini Magharibi umbali wa km 60 kutoka Halmashauri ya wilaya Kyerwa. **Shule yetu ina mazingira bora ya kufundishia pamoja** na **kujifunzia yanayo mwezesha mwanafunzi kujifunza kwa ufanisi .**
.

**USAFIRI .**

**Namna ya kufika shuleni**, Ukitokea Manispaa ya Bukoba unaweza kupanda Bus au Hiace kutoka Bukoba hadi Karagwe , na utashuka sehemu inayoitwa **Kayanga Nauli tsh 6,000/=** , au ukitokea Benaco utashuka Omurushaka , panda

TAX zinazoenda Kayanga Nauli tsh **1000**/= , Ndipo utapanda Hiace zinazotoka Kayanga kwenda Bugomora , Nauli tsh 10,000 /= na utafika shuleni moja kwa moja , na utashukia { Nyamiyaga / kwa Museveni }.

N.B : - Wahi kufika standi ya kayanga kabla ya saa nane za mchana ili uweze kupata magari ya kukufikisha shuleni moja kwa moja .

**Muhula wa masomo utaanza tarehe ………... Hivyo, mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ………….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe ………... Na mwanafunzi atapokelewa kwa muda wowote atakaofika shuleni kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi. Baada ya muda wa kuripoti kuisha hakuna mwanafunzi yeyote atakayepokelewa bila ya kutoa taarifa kabla kwenye uongozi wa shule .**

**2 .MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA :-**

**2.0 SARE YA SHULE .**

i. Sketi mbili ndefu zinazoishia kwenye kifundo cha mguu **{ Rangi ni Dark blue }** aina ya mshono **RINDA BOX** { Rinda tatu mbele na rinda tatu nyuma {**Tafadhari zingatia vipimo vya urefu wa sketi }**

ii. Shati mbili nyeupe aina ya tetron mikono mirefu.

iii.Viatu vya shule ni vyeusi vyenye kamba { vyenye visigino vifupi} jozi mbili .

iv. Soksi nyeupe jozi mbili ndefu {stocking } na soksi nyeusi ndefu kwa ajili ya jioni / Usiku

v. Tai yenye michirizi mieusi na mieupe yenye nembo ya shule .

vi.Sweta ya shule yenye rangi ya kijivu na yenye nembo ya shule na Jaketi 01 nzito nyeusi T isiyo kuwa na alama yoyote kwa ajili ya kujikinga na baridi wakati wa usiku .

vii.T-shirt ya dark blue yenye nembo ya shule

viii.**Kwa waislam wanaweza kushona suruali mbili zisizobana , Hijabu 02 {kijuba} iwe ni tetron nyeupe ifunike kifua , ifike kwenye kifundo cha kiganja , ndefu usawa wa mikono ya shati .**

**2.1 SARE ZA MICHEZO**:-

(i) Pedo / Bukta ya njano.
(ii) T-shirt moja rangi ya njano.
(iii) Viatu aina ya raba jozi moja.
(iv) Soksi ndefu za michezo.
(v) Tracksuit rangi ya blue

2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI :-

**2.2.1 VIFAA VYA DARASANI :-**

i. Daftri kubwa 12 (counter book 4 quire)
ii. Kalamu za wino za kutosha
iii. Graph pad 1 ya karatasi yenye kurasa 50
iv. Kasha la vifaa vya hesabu (Mathematical Set) na rula 1
v. Dissection Kit
vi. Daftari ndogo 10 za kufanyia mazoezi darasani.
vii. Scientific Calculator {Casio Fx 991 orginal }
viii. Mfuko kwa ajili ya kubebea vifaa vya taaluma

i x) Kila mwanafunzi aje na vitabu vya vya masomo ya tahasusi yake husika , iwe PCB au CBG (orodha imeambatanishwa)

2.2.0 **MAHITAJI BINAFSI YA BWENINI**:-

Mzazi atamnunulia mahitaji binafsi mtoto wake kama ifuatayo:-

1. Gauni mbili zenye rangi ya light blue zisizobana **solo** kwa ajili ya kushindia baada ya muda wa darasani .
2. Shuka pair 2 rangi ya ( blue ) , taulo / Kanga , Night dress .
3. Godoro dogo futi 2½ x 6 , Mto, Blanket na Chandarua nyeupe .
5. Sanduku imara la mbao au chuma lenye kufuli, taa ya solar isiyo na mwanga hafifu kwa tahadhali
6. Vyombo vya chakula {Sahani , bakuli , kikombe na kijiko }
7. Mswaki na dawa ya meno, Nguo za ndani za kutosha , Kitana , Ndala au yebo .

8. Mafuta ya kujipaka, brush ya viatu, dawa ya viatu, toilet paper 5pcs, Taulo za kike Pcs 5, sabuni za kuogea na kufulia, soap dish ,vibanio vya nguo ,
9. Ndoo ndogo 1 ya Lt 10 kwa ajili ya kutunzia maji yake , beseni 1 kwa ajili ya kuogea na kufulia
10. Chupa ya kuhifadhia maji ya kunywa .

***NB: Mwanafunzi yeyote hataruhusiwa kuwa na nguo nyingine tofauti na sare za shule zilizoelekezwa hapo juu*.**

### 2.2.2 MAHITAJI MENGINE:-

i. Ndoo 1 ya Lt 20, kotama 1, Mfagio wa ndani { soft bloom } 1 , Mopper { 01 }
ii. Box file (Ni lazima) kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu zake mwenyewe
iii. Karatasi (ream $A_4$ 2 ) kila muhula
iv. Fedha za matumizi yake binafsi { Pocket Money }
v. Mwavuli 1 na viatu vya mvua
vi. Koti la maabara 01

### 2.3 **MICHANGO MBALIMBALI :-**

Mwanafunzi anatakiwa kulipiwa michango mingine kabla ya kuripoti shuleni kama ifuatavyo:-

| S/N | AINA YA MCHANGO | KIASI (TSHS) |
|---|---|---|
| 1 | Uendeshaji wa shule | 65,000 /= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| **JUMLA** | | **80,000/=** |

**MUHIMU**: -

Fedha hizi zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. **31 90 11 00 065** katika Benki ya NMB tawi lolote. Jina la akaunti ni **NYAMIYAGA SECONDARY SCHOOL RECCURENT ACCOUNT.** (Tafadhali andika dhumuni la malipo na jina la mwanafunzi kwenye Pay in slip). Shule haitawajibika kwa atakayelipa fedha **taslimu kwa mtu yeyote yule**.

Kila mwanafunzi ajiunge na mfuko wa **BIMA YA AFYA NHIF** na aje na Kitambulisho cha Bima shuleni.) Kwa suala la matibabu, shule inatoa huduma ya kwanza tu na mwanafunzi akihitaji matibabu zaidi **mzazi wa mwanafunzi husika atagharimia matibabu yake.**

**TAALUMA** .

Mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote darasani na **kufanya kazi/ mazoezi** yote atakayopewa na walimu wake pamoja na **majaribio mbalimbali** . Na asipo fanya hivyo ataadhibiwa na hata kurudishwa nyumbani kwa kosa hilo. Mwanafunzi pia anatakiwa kupata alama kuanzia **50 /100** kwa kila somo wakati wa mtihani wa kufunga muhula na mwaka na akishindwa kufikisha alama hizo hataruhusiwa kwenda likizo .

## 3.Sheria na Kanuni muhimu za Shule :-

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
ix. Kutunza mali za shule.
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Akiwa shuleni , mwanafunzi atatumia simu zilizoidhinishwa na uongozi wa shule kwa ajili ya kuwasiliana na mzazi / mlezi pale itakapo kuwa na uhitaji .**

- **Mwanafunzi atakaye kamatwa na simu , laini {SIM CARD } ,Chaja au kifaa chochote chenye viashiria vya simu atarudishwa nyumbani mara moja na siku ya kurudi shuleni atalazimika kulipa faini ya tsh 200,000/= ambayo italipwa kupitia kwenye account ya shule .**

- **Hatua hii imewekwa kwa ajili ya kulinda nidhamu na kuhakikisha utaratibu huu unazingatiwa kikamilifu shuleni .**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi.
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa.
x. Kusababisha mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

xvi. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule .

**Hakikisha viambatanisho vyote vinavyotakiwa kujazwa vimejazwa kwa usahihi na kukabidhiwa shuleni wakati wa kuripoti**.

**5**.**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB**: - Mwanafunzi anapokuja kuripoti shuleni aje na :-

. Cheti za kuzaliwa { photocopy }

.Result slip { photocopy } ya kidato cha nne

.Mhamiaji aje na matokeo ya shule alikotoka .

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**.....................**
**ABEDNEGO G.NDIBALEMA**
**MKUU WA SHULE**

**ANGALIZO: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0767 58 36 40 /0782 72 60 96**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0746 815 553 / 0682 088 192**
- **Mwandamizi Taaluma:   0675993 077 / 0625 101 121**
- **Mwandamizi Malezi: 0621 430 421 /0756 361 627**

**MAELEZO YA MWANAFUNZI KUHUSU TAALUMA**

.Malengo yangu katika kufaulu mitihani ya masomo nitakayo yachukua ya PCB / CBG ni kama ifuatavyo :-

| MASOMO | ALAMA / GRADE | |
|---|---|---|
| 1.PHYSICS | ………….. | …………… |
| 2.CHEMISTRY | …………. | ………….. |
| 3.BIOLOGY | …………. | ………….. |
| 4.BAM | ………….. | …………. |
| 5.GENRAL STUDIES | ……………. | …………….. |
| 6. GEOGRAPHY | …………… | ………….. |

.Mikakati yangu ili kufikia malengo hayo :-

……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..

.Nikishindwa kufikia malengo malengo yangu nini kifanyike ?

……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..
……………………………………………………………………………………………………………………………………..
…………………………………………………………………………………………………………………………………

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………..mzazi/mlezi wa …………………nimezisoma sharia za shule nikiwa na mwanangu na kujadili pamoja naye na amezielewa. Ninakubaliana kushirikiana na uongozi wa Shule katika malezi ya mwanangu na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na uongozi wa shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya sheria na kanuni hizi.

Saini ya Mzazi/mlezi.......................................tarehe....................Na.ya simu…………………………

**AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi .........................................wa kidato cha ................... nimesoma kwa makini sheria na taratibu za Shule nikiwa na mzazi/mlezi wangu. Nimejadiliana naye na nimeelezwa vizuri kabisa. Ninaahidi kuwa nitazifuata na endapo nitakiuka mojawapo ya sheria na taratibu hizi hatua zichukuliwe dhidi yangu. Ewe mwenyezi Mungu nisaidie.

Saini ya mwanafunzi...........................................Tarehe ......................

Ni imani yangu kuwa utafuata hizi sheria ili uweze kujifunza kwa bidii na kwa mafanikio yaliyo bora.
Nakutakia kila la heri na karibu sana Nyamiyaga Sekondari.

...............................................
ABEDNEGO G.NDIBALEMA
**MKUU WA SHULE**

***KIAMBATISHO B***

*Shule ya Sekondari Nyamiyaga*

*S. L. P 592, Kyerwa. Simu: 0782 72 60 96*

Barua pepe: **nyamiyagasecondary@gmail.com**

**MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina la Mwanafunzi............................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ..........................................................................
3. Mahali alipozaliwa: Mkoa ................................ Wilaya......................................
   Tarafa....................................Kata ...............................Vijijini/mtaa...............
4. Dini....................................... Dhehebu.......................................................
5. Jina la baba mzazi/mlezi.........................................................................
   Anuani.......................................... Namba ya simu.......................................
   Kazi ya baba mzazi/mlezi...................................................
   Yuko hai? Ndiyo/ Hapana (kata isiyohusika)

6. Jina la mama mzazi/mlezi…..................................................Anuani ................................ Namba ya simu...........................................kazi ya mama mzazi/mlezi.................................................
   Yuko hai? Ndiyo/hapana (kata isiyohusika)

| ***Picha ya baba mzazi/mlezi*** | ***Picha ya mama mzazi/mlezi*** |
| --- | --- |

7. Ndugu wa karibu aliyeridhiwa na mzazi/mlezi anayeweza kupewa taarifa za matatizo ya mwanafunzi kwa haraka endapo mzazi/mlezi hatapatikana.
   Jina kamili........................................................Anuani...................................
   Namba ya simu.....................................................
   Kazi yake …..............................................uhusiano na mwanafunzi.............................................

***Picha ya ndugu wa karibu***

***KIAMBATISHO C***
**MEDICAL EXAMINATION FORM**

**NAME OF STUDENT....................................................................**

To medical officer **I/C** of
.........................................................District/ Regional/Referral/Designated Hospital,
**P.O BOX**.........................................

**Please examine the above named in full as to her physical and mental fitness for being able to pursue two years of Secondary School Education. In case of an acute Defect / disability in each category or subcategory may render the applicant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs:-**

i. Blood pressure........................................................................

ii. Sickle cell test.......................................................................

iii. (a) Eye sight...........................................................................

(a) Spleen.........................................................................

(b) Hearing........................................................................

(c) Veneral diseases.........................................................

(d) Lepsory..............................................................................

(f) Typhoid.........................................................................

iv. Neuroses...............................................................................

v. Other serious disease ....................................................................

General comment(s).....................................................................................

Name..........................................................................................................
Designation..................................................................................................
Official stamp................................................... Date.............................................

**ANGALIZO**: mzazi athibitishe kuwa vipimo hivi vimefanyika kikamilifu na siyo kujaza jina na saini ya Mganga. Atakayegundulika kuwa hakuchukua vipimo kihalali atarudishwa

nyumabani.

***KIAMBATISHO D***

*Shule ya Sekondari Nyamiyaga*
*S. L. P 592, Kyerwa. Simu: 0620 670 252/0782 7260 96*
Barua pepe: **nyamiyagasecondary@gmail.com**

**FOMU YA KUKUBALI NAFASI**

Mimi..............................................nakubali nafasi ya kidato cha tano niliyopewa na Shule ya Sekondari Nyamiyaga . Ninaahidi kutii na kufuata kwa uaminifu sheria na taratibu zote za shule, kujifunza kwa bidii, juhudi na maarifa kwa uwezo wangu wote ili kutimiza lengo la kufaulu kwa kiwango cha juu kwa faida yangu, familia yangu na Taifa kwa ujumla. Ninaahidi kuripoti shuleni siku iliyopangwa bila kuchelewa.

Saini ya mwanafunzi.........................................................
Tarehe ..........................................................................

**MKATABA WA KUTOSHIRIKI MIGOMO NA FUJO /VURUGU .**

{Fomu hii ijazwe na kurudishwa shuleni }

Mimi …………………………………………………………………………………………………………..ambaye ni mwanafunzi wa kidato cha ……………………………….katika shule hii, naahidi kutojihusisha kwa namna yoyoye ile katika migomo , fujo , au kosa lolote la Jinai ambalo litahatarisha Amani au litakalo kuwa kinyume cha Sheria , Kanuni na Taratibu za shule .

Endapo ikithibitika kuwa nimetenda kosa au makosa tajwa hapo juu sitakuwa na pingamizi juu ya hatua za kinidhamu zitakazo chukuliwa dhidi yangu .

Jina la mwanafunzi …………………………………………………
Sahihi ya Mwanafunzi ……………………………………………
Tarehe …………………………………………………………

Jina la Mzazi/ Mlezi ………………………………………………
Sahihi ya Mzazi / Mlezi ……………………………………………
Tarehe ……………………………………………………………………

**AHADI YA MZAZI /MLEZI**

Mimi mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………………………………………………………

Na ahidi kumhimiza mtoto wangu kusoma kwa bidii , kulipa michango yote ya shule , kufuatilia maendeleo yake kitaaluma ikiwa ni pamoja na maelekezo mengine yatakayo tolewa na uongozi wa shule .

Jina la Mzazi / Mlezi ………………………………………………….. Sahihi ya Mzazi /Mlezi ………………………………………

**FOMU YA KURIPOTI SHULENI**
**SHULE YA SEKONDARI NYAMIYAGA**

i.Tarehe ya kuingia shuleni ………………………………Admission No………………
ii.Jina la mwanafunzi ……………………………………………………………………
iii.Darasa na Mchepuo anaoingia ………………………………………………………………
iv.Kabila …………………………………………………………………………………………………
v.Tarehe ya kuzaliwa…………………………… Wilaya ………………………………………
vi.Jina la baba/ Mlezi ……………………………………………………………………………..
vii.Kazi ya baba/ Mlezi ……………………………………………………………………………
viii.Namba ya simu ya baba/ Mlezi ……………………………………………………………
ix.Mahala baba /Mlezi anapoishi ……………………………………………………………………..

**ORODHA VITABU VYA VITABU**

| SUBJECT | BOOK TITLE |
|---|---|
| 1. **PHYSICS** | 1. Advanced Level Physics by Nelkon & Parlker 7th edition |
| | 2. Principles of Physics - TOM DUNCAN |
| | 3. A' Level Physics - Roge Municaster { 4th Edition} |
| | 4.S.Chands Principals of Physics for class XI & XII<br>5.Comprehensive Physics { Volume 1 }<br>6. Comperensive Physics { Volume 2} |
| **2.CHEMISTY** | 1. Inorganic part 1 & II by TIE |
| | 2. Physical Chemistry - Mzumbe book project |
| | 3.Chemistry part 1 , Text book for class XI {S.Chands }<br>4.Chemistry part 2, Text book for class xii { S. Chands }<br>5.Advanced Chemistry 1 review { problems and solutions } |
| | 6.Chemisry for A LEVEL { Fourth Edition } by RAMSDEN<br>7.Conceptual Chemistry class XI by S .Chand<br>8.Conceptual Chemistry class XII by S. Chand<br>9..Advanced Chemistry 2 review { problems and solutions<br>10.0rganic Chemistry part A &B { Mzumbe BK project |
| 3. BIOLOGY | 1. Advanced Biology for Secondary Schools – Michael R.<br>2.Verma P.S and Pandey P.B { 2010} S. Chands for class XI<br>3.Cell Structure and Organization – L . Msaki<br>4.Taylor el al { 2006}Biological Science , third edition , Cambriadge University Press.<br>5.Glenn and Toole S. {1999}, Understanding Biology for Advanced Level , fourth edition<br>, Stanlet Thornes Publishers Limited .<br>6.Verma P.S and Pandey P. B { 2006} S.Chands for class XI , first edition, India, S.Chands<br>and Campany Limited. |
| 4. BASIC APPLIED MATHEMATICS {BAM } | 1. Basic Applied Mathematics { BAM } for Advanced level Secondary Schools , Student's book Form 5 & 6 .<br>2. Any other book authorized by TIE . |
| 5. GENERAL STUDIES | 1. General Studies For Secondary School - By Mbalase, R. General Studies by SETA . |

| | |
|---|---|
| | 2. Bigirwamungu, J. & Deogratius S.M (2012) Understanding Advanced Level General Studies: Advanced Level Secondary Schools, |
| | 3. Nyangwine, C.M, Bukagile G.R & Maluka S.O (2010) Contemporary Approach for Advanced Level: General Studies Notes form 5 & 6. |
| | 4. General Studies By SETA |
| | 4. General Studies, Supplementary Book for Advanced level and Colleges , Second Edition – Konrad Adenaker Stiftung |
| 6 GEOGRAPHY | 1. Principles of physical Geography - F.J Monkhouse |
| | 2.Physical Geography for Secondary Schools -D.T Msabila |
| | 3.Landforms in Africa - Collin Buckle |
| | 4'Humana and Economic Geography Advanced Level – DT. Msabila |
| | 5Geography : An Intergrated approach - David Waugh |
| | 6.Human and Economic Geography – Goh Cheng Leong<br>7.Practical Geography for Africa – John M. Richard |
| | 8 .Practical Geography for A – Level - Francis Mnyawi<br>9.Research Methodology , Methods and Techniques – C.R. Kothari<br>10. Physical Geography for Advanced Level Secondary Schools F 5 & 6 { TIE }<br>11.Human Geography for Advanced Secondary Schools F5 &6 { TIE }<br>12.Practical Geography for Advanced Secondary Secondary Schools F 5 & 6 { TIE } |

**TAFADHARI NUNUA VITABU VISIVYO PUNGUA ANGALAU VIWILI KUTOKA KILA SEHEMU NA VITAKAGULIWA WAKATI WA KURIPOTI SHULENI .**